

A Ufunuo na uvuvio. 1 Petro 1:10-11.

- ❖ Ufunuo ni maarifa ambayo Roho mtakatifu huyapatiliza kwetu kuhusu mambo ambayo hatuwezi kuyaelewa wenyewe.
- ❖ Uvuvio ni namna Roho Mtakatifu anavyoeleza ukweli kupitia kwa wanadamu.

B Roho Mtakatifu na chimbuko la Neno:**❖ Mfunuaji. 1 Wakorintho 2:10.**

- Tungejuaje mapenzi ya Mungu kama Roho Mtakatifu asingekuwa ametufunulia katika neno?
- Kweli za Biblia ni ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Sio mawazo wala tafsiri za mwanadamu bali ni za Mungu.

❖ Mvuviaji. 2 Petro 1:21.

- Mungu aliwaaongoza kuelezea mawazo yake katika namna ambayo ni thabiti na ya kuaminika kwa kutumia maneno yao yaliovuviwa.
- Mchakato wa uandishi ulitofautiana toka mtu hadi mtu na wakati hadi wakati.
 - (a) Wakati mwingine walipokea maneno kama yalivyo yakitangulia na “Bwana asema hivi” (Isaya 37:6).
 - (b) Wakati mwingine waliona maono na njozi walizozielezea kwa maneno yao (Ezekieli 1:4).
 - (c) Wakati mwingine walichunguza na kutafiti ili kuelezea kweli na kuzifundisha kwa usahihi (Luka 1:6).

❖ Mkweli. Zaburi 119:160.

- Baadhi ya watu hutilia shaka kuwa Biblia ni ya kweli kwa sababu hawa kukuelewa kilichomo au hawa kukubali kweli za miujiza zilizomo.
- Mungu hasemi uongo (Waebrania 6:18). Kwa hiyo, Kila alichosema kupitia neno lake NI KWELI.
- Hatuwezi kuihukumu Biblia; Mawazo yetu yapaswa kuhukumiwa nayo (Biblia).

C Roho Mtakatifu na Neno leo.**❖ Mwalimu wetu. Yohana 16:13.**

- Hatuwezi kuelewa kweli za Biblia kwa akili zetu, kwa sababu kweli za kiroho lazima zieleweke kiroho (1 Wakorintho 2:13). Ndiyo maana Roho Mtakatifu hutusaidia:
 - (a) Kuekewa ukweli wa kimaandiko wa Biblia.
 - (b) Kuelewa ukweli kuhusu sisi.
- Tunapoamua kuitikia uongozi wa Roho Mtakatifu na kwa unyenyekevu tunakubali maelekezo ya Mbingu yaliyo katika Biblia, Maisha yetu hubadilishwa kwa neema ya Mungu, na akili zetu hulidwa dhidi ya udanganyifu wa Ibilisi.

❖ Hakuna mkanganyiko. Yohana 5:46-47.

- Je; Roho Mtakatifu anaweza kutuongoza katika ukweli unaomuhusu Yesu (au fundisho lingine lolote) unaopingana na ujumbe mwingine wa Biblia (Yohana 16:13-14)?
- Roho Mtakatifu hawezi kupingana na neno la Mungu. Kama mtu akisema amevuviwa na Roho Mtakatifu lakini anafundisha mafundisho yanayopingana na Biblia, Basi huyo hasemi ukweli.